<table>
<tr><th colspan="2">HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA MUONOGOZO WA KATIBA YA VIKUNDI.</th></tr>
<tr><td>1.</td><td>TAARIFA ZA KIKUNDI
<ul>
<li>Jina la kikundi.</li>
<li>Mahali kikundi kilipo.Taja kata na Mtaa/kijiji.</li>
<li>Anwani ya kikundi.Taja:<br>- Namba ya simu ya viongozi<br>- sanduku la posta kama lipo la kikundi au kijiji au lolote<br>Ambalo kikundi kinaweza kupata taarifa.<br>- barua pepe au fax.nk</li>
</ul></td></tr>
<tr><td>2.</td><td>MADHUMUNI YA KIKUNDI.<br>Kikundi lazima kiorodheshe shuguli na mambo ambayo kitahusika kuyafanya:
<ul>
<li>Kwanini wameanzisha kikundi.</li>
<li>Shuguli watakazo zifanya baada ya kuanzisha kikundi.</li>
<li>Mfano: shuguli hizo zinaweza kuwa kama;<br>- Kuweka Akiba na kukopeshana.<br>- kuendesha biashara ndogondogo katika ngazi ya mtu mmoja mmoja au kikundi kulingana na makubaliano ya kikundi..<br>- Kugawana faida mwisho wa mzunguko.<br>- kuwa na mfuko wa jamii au bima ya kikundi (Elimu hii itatolewa kuvifanya vikundi kuwa endelevu).
<ul><li>Kuuza na kununua hisa .nk.</li></ul></li>
</ul>
ANGALIZO: Shuguli nyingine ambazo kikundi kitapendelea ziwekwe a zinaweza kuwa tofauti na zilizo tajwa hapo juu kama mfano tu.</td></tr>
<tr><td>3.</td><td>UANACHAMA:
<ul>
<li>Umri wa mwanachama kujiunga na kikundi.tunashauri uanzie miaka 15 nakuendelea.</li>
<li>Sifa nyinginea ambazo wanakikundi wanapenda wanakikundi wenzao wawe nazo.<br>Mfano: Muadilifu,akili timamu,anafahamika na nyingine.</li>
</ul></td></tr>
<tr><td>4.</td><td>WAJIBU WA WANAKIKUNDI:
<ul><li>Taja wajibu wa wanakikundi.</li></ul></td></tr>
<tr><td>5.</td><td>HAKI ZA WANAKIKUNDI :<br>Elezea haki nambazo mwanakikundi atazipata akiwa mwanakikundi wa kikundi husika.</td></tr>
<tr><td>6.</td><td>UKOMO WA MWANAKIKUNDI/MWANACHAMA.<br>Ukomo wa mwanachama unaweza kutokea kwa sababu tofauti, ni muhimu kulingana na kikundi kitakavyoamua au mazingira waliyoyataja inaweza kuwa kwa kwakujitoa,kufukuzwa au kifo.
<ul><li>KWAKUJITOA: Inawezekana mwanakikundi akaamua kujitoa katika kikundi kwa sababu mbali mbali ambazo ni:<br>(i) KUWA NA SABABU MAALUM. kikundi kitaje kanuni na hatua gani kitachukua kwa mwanakikundi kumpatia haki yake na stahiki zake.<br>-Kujitoa kwa sababu za msingi na hana deni. kikundi kitaje taratibu gani itachukuliwa:<br>- Kujitoa kwa sababu za msingi na ana deni. kikundi kitaje taratibu gani itachukuliwa:</li></ul></td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| | (ii) **KUTOKUWA NA SABABU.**kikundi kitaje kanuni na hatua gani kitachukua kwa mwanakikundi kumpatia haki yake na stahiki zake .<br>- Kujitoa bila sababu za msingi asipokuwa na deni: kikundi kitaje ni jinsi gani kitampatia haki yake.<br>- Bila sababu za msingi na anadaiwa na kikundi.<br><br>• **KUFUKUZWA.** Kikundi kitaje sabababu za mwana kikundi kufukuzwa au kujifukuza kwenye kikundi kulingana na makubaliano yao.<br>• **KIFO:**Nisababu ambayo haizuiliki. |
| **7.** | **KUFUKUZWA UANAKIKUNDI/UANACHAMA:** Kikundi kitaje sababu za kufukuzwa mwanakikundi. |
| **8.** | **KAMATI YA UONGOZI**<br>Kikundi kitakuwa na Kamati ya Uongozi itakayoundwa na viongozi wafuatao:<br>- Mwenyekiti<br>- Katibu<br>- Mhasibu /mtunza hazina.<br>- Wahesabu pesa wawili/ cashiers. |
| **7.** | **KAZI ZA VIONGOZI** |

## KAZI ZA VIONGOZI

| WAJIBU WA MWENYEKITI |
|---|
| • Kuitisha mikutano, kusoma ama kutaja agenda na kuongoza majadiliano<br>• Kutunza nidhamu na kuwatoza faini wanaokosea kama inavyotakiwa katika katiba hii.<br>• Kuhakikisha kuwa mikutano inafuata utaratibu sawasawa (hasa taratibu za mfuko wa jamii, kuweka akiba na kutoa mikopo) na katiba inafuatwa na inaheshimiwa.<br>• Kukiwakilisha kikundi kwa watu wa nje na kwa wasio wanachama. Kama ikihitajika atatoa historia ya kikundi na utendaji kazi wake.<br>• Kuendesha majadiliano ya maswala yanayojitokeza katika mkutano mkuu na kuhakikisha kuwa mawazo ya kila mtu yanasikilizwa.<br>• Kuwezesha kufikia muafaka katika migogoro kati ya wanachama kwa njia ya amani. |
| **MAJUKUMU YA KATIBU WA KIKUNDI** |
| • Kuhakikisha kuwa miamala yote ya fedha inayohusu Mfuko wa Jamii, akiba na mikopo inafanyika mbele ya wanachama wote katika utaratibu unaokubalika na kwa kupitia wahesabu fedha<br>• Kuandika kumbukumbu zote za Mfuko wa Jamii, Akiba, Adhabu, Mikopo na fedha taslim katika daftari<br>• Kugonga mihuri katika vitabu vya wanachama.<br>• Kutoa muhtasari wa mahesabu ya fedha ya kikundi katika kila mkutano nk. |

| | |
|---|---|
| | **MAJUKUMU YA MTUNZA HAZINA**<br>• Kutunza kumbukumbu zote za fedha za kikundi,<br>• Kugonga mihuri vitabu vya wanachama na kutunza sanduku la fedha nyumbani kwake<br>• Kuleta sanduku la fedha ambalo pia lina kumbukumbu zingine ndani, katika kila mkutano wa wanachama wote. |
| **8.** | **UCHAGUZI WA VIONGOZI.**<br>• Muda wa kiongozi kukaa madarakani.<br>• Uchaguzi utafanyika kila baada ya muda gani.<br>• Jinsi gani uchaguzi utakuwa unafanyika.<br>• Idadi ya majina yatakayo pitishwa.<br>• Upigaji wa kura uwe wa siri au wazi. |
| **9.** | **UKOMO WA UONGOZI.**<br>▪ Kikundi kitaje ni sifa zipi zitawafanya viongozi waondolewe madarakani |
| **10.** | **MIKUTANO YA KIKUNDI:**<br>▪ Kikundi kitaje watakutana maranapi kwa mwezi kulingana na makubaliano yao? |
| **11** | **KUFARIKI KWA MWANAKIKUNDI.**<br>Lazima kikundi kieleze vigezo vifuatavyo:-<br>▪ Watu watakao changiwa kwa aliyefariki au aliyefiwa.<br>▪ Mchango wa mfiwa utakuwa kiasi gani?<br>▪ Nani atakaye changiwa?<br>▪ Rambi rambi au michango itatokana na nini? |
| 12 | **ADHABU KWA MAKOSA MBALIMBALI:**<br>**i.** Kuchelewa kikao bila kutoa taarifa hatachangia shilingi ngapi?<br>**ii.** Kutokuhudhuria kikao bila taarifa faini shilingi?<br>**iii.** Kutoka kwenye kikao baada ya kuchangia mfuko wa jamii na kununua hisa faini ni shilingi ngapi?<br>**iv.** Kuongea bila idhini ya Mwenyekiti faini shilingi?<br>**v.** Kuonesha dharau faini shilingi?<br>**vi.** Kiongozi asipotenda kazi yake vizuri faini shilingi?<br>**vii.** Mtu mchonganishi na mgomvi atapigwa faini ya shilingi ngapi?<br>**viii.** Ukichelewesha mkopo utatoa asilimia ngapi ya mkopo huo kama adhabu. Lakini utatakiwa kurejesha mkopo na riba yake ndani ya wiki moja kabla uamuzi wa kukatwa hisa haujatekelezwa.<br>**ix.** Mlio wa simu yako ukisikika wakati wa kikao utalipa faini **shilingi?** |
| **13** | **HUDUMA ZITOLEWAZO NA KIKUNDI**<br>• AKIBA<br>▪ Thamani ya hisa au michango/Ada ya kikundi Kima cha chini na cha juu?<br>▪ Itafanyika kila baada ya muda gani kulingana na kikundi kilivyopanga |

| | |
|---|---|
| | • MIKOPO.<br>▪ Anayestahili kukopa ni mwanakikundi mwenye sifa gani?.<br>▪ Muombaji atatakiwa angalau awe amechangia michango kiasi gani?<br>▪ Kiasi cha chini cha kukopa ni shilingi ngapi?<br>▪ Muda wa kukaa na mkopo inatakiwa iwe muda gani?<br>▪ Riba ya mkopo ni asilimia ngapi kwa mwezi?<br>▪ Mkopo urejeshwe kwa muda gani?<br>▪ Ili kupewa mkopo mkubwa mwanakikundi awe na wadhamini wangapi?.<br>▪ Je mwanakikundi anaruhusiwa kuchukua mkopo mara gnapi endapo ameishakopa |
| **14** | **MFUKO WA JAMII.**<br>▪ Kikundi kitaje kitachangia Mfuko wa Jamii kila baada ya muda gani waliopanga kuchangia Ada au Michango ya kikundi?<br>▪ Mfuko huu utachangiwa kwa muda gani na kuaanza kutumika?<br>▪ Kila mwanakikundi atachangia shilingi ngapi?<br>▪ Mfuko utasaidia majanga ya aina gani? Mfano: Vifo, moto, Magonjwa na kuibiwa.<br>▪ Kikundi kitaje Watakaohudumiwa na mfuko huu katika familia ya mwanakikundi ni: mwanakikundi mwenyewe, mwenzi wa ndoa, watoto wa mwanakikundi, wazazi wa mwanakikundi na mtu mwingine ambaye mwanakikundi anaishi naye.<br>▪ Je Kikundi kitahudumia mgonjwa mara ngapi tu kwamuda watakaopanga?.<br>▪ **Vifo**: Kama mwanakikundi atafiwa na mume, mtoto, mzazi au mtu mwingine anayemtegemea kikundi kitachangia kiasi gani? Kama rambi rambi?<br>▪ Majanga ya kuuguliwa mwanakikundi hatachangiwa silingi ngapi?<br>▪ Misaada mingine itakayotolewa na mfuko huo niya aina gani?<br>▪ Iwapo mwanakikundi akifanya udanganyifu kuhusu vifo au magonjwa, kikundi kita mchukulia hatua gani?<br>**ANGALIZO:** Vikundi vingi vilivyofanikiwa vimetumia mfumo huu kufikia malengo yao na kukabili matatizo na majanga yasiyo zuilika.tungeshauri kikundi kutumia mfumo huu kupunguza gharama zisizo za lazima wakati wa matatizo yanapo wakuta wanakikundi. |
| **15.** | **MWISHO WA MZUNGUKO KUGAWAWANA FAIDA/ KUVUNJA KIKUNDI:**<br>**A:Mwisho wa mzunguko:** ni muda ambao kikundi kimekubali kujiendesha kwa kuweka na kutoa mikopo kwa muda walio panga ambapo kikundi kitaweka<br>• Hapa kikundi kinafikia mwisho wa mzunguko kwa kugawana hisa zao na faida kwa muda walio kubaliana.<br>• Wanakikundi wanakubaliana kama wataacha hisa anzia au watagawana fedha zote.<br>• Kikundi kinaweza kuingiza watu wapya na kuweka hisa mpya au ada mpya.<br>• Wanakikundi wanaotoka kwenye kikundi wafahamike na maombi mapya ya usajili yafanyike.<br>B. **Kuvunjika kikundi/ukomo:**hapa inaweza kuwa<br>• Kikundi hakitaendelea na shuguli za kikundi<br>• Kikundi kinavunjwa kukosekana kutokuwa na uaminifu na sababu watakazo zitaja.<br>• Kikundi kitowe kinatakiwa kitowe taarifa kwa Afisi ya Maendeleo ya jamii kiondolewe kwenye orodha. |

16. **MABADILIKO YA KATIBA:**

Endapo litajitokeza jambo lolote ambalo halikuguswa na katiba hii, lakini likawa na maslahi kwa kikundi, basi Mkutano Mkuu wa wanakikundi wote utalijadili na kulitolea maamuzi. Na uamuzi utakaotolewa, utajumuishwa katika katiba hii kama kipengele.

17. **IDHINI**

Katiba hii baada ya kutungwa na wanakikundi wenyewe na baadaye kuchapwa, imesomwa na kukubaliwa na wanakikundi. Pia ithibitishwe kwa kusainiwa na katibu na Mwenyekiti.

18. **ORODHA YA MAJINA: Mfano wa jedwali lla majina ya wana kikundi.**

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA | SAHIHI |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |

SUSTAINABILITY OF MSLAs (MTAA SAVING AD LOAN ASSOCIATIONS)

Vikundi vingi vya kuweka na kukopa vimeshindwa kuwa endelevu kutokana na utafiti uliofanyika na CARE international changamoto ya kutokuwa endelevu na mafanikio sababu kubwa ni:

- **Kukosa elimu ya fedha**. Financial Education Training (FET)
- 
- Ambayo ni msaada kufikia malengo na kuwa na matokeo makubwa.Ambayo.
- **Mfumo wa duni uendeshaji vikundi**.vya kuweka na kukopa na uzalishaji mali. Ambapo vikundi vingi vinatumia njia ya kienyeji kuendesha vikundi kwa kuchangishana Ada.kwa mwezi au kwa wiki inayo lingana kwa wana kikundi japo mapato yanatofautiana ambayo upelekea kutokuwepo tofauti kati yake na vikundi vya Rotating and saving credit Association(ROSCA)
- **Kuwa na riba kubwa**. kama ya taasisi kukopesha 10%
- **Ukosefu wa elimu ya ujasiliamali na uzalishaji mali**,*Income generating Activities* (**IGA).**

**HIYO IMEPELEKEA CHANGAMOTO ZIFUATAZO KWA ASILIMIA KUBWA YA VIKUNDI VILIVYO SAJILIWA KUTOKUWA ENDELEVU:**

- Kukosa vigezo vya kupewa mikopo na Taasisi za kifedha(Benki) na Taasisi za mikopo.
- Mitaji kuwa duni.
- Urejeshaji wa mikopo kuwa duni.(Manispaa kupitia mfuko wa wanawake na vijana)
- Hamasa ya watu kujiunga kuwa duni.
- Kupungua kwa vyanzo vya mapato ya ndani ya manispaa.

**NINI KIFANYIKE HILI KUFIKIA MALENGO YA VIKUNDI ENDELEVU:**

Mfumo wa vikundi katika ulimwengu wa nchi zinazoendelea umebadilika kwa kutumia mfumo unaojulikana kama VSLAs. Ambao ni mfumo rafiki na unafaa kwa watu wa kipato cha chini kujitengenezea mitaji na kuweza kuitawala fedha kufikia malengo yao.

Mfumo huu umetumiwa vizuri na mashirika yasiyo ya kiserikali kama CARE international kwenye nchi ya Srilanka, India, Pakistani na Tanzania chini ya CARE INTERNATIONAL na PACT.

**KWANINI VSLAs (Village saving and Loans Associations)**


Kwanini VSLAs ni mfumo unaoleta tija na vikundi endelevu, kama ukitumiwa vizuri na vvya kuweka na kukopa pamoja na uzalishaji mali?

:Misingi mikuu ya VSLAs kufanikisha Vikundi endelevu vya uzalishaji mali:

1. Elimu ya Fedha yenye mada kumi na sita(FET) Ambazo ni.
    - Kuweka vipaumbele vya fedha.
    - Kuweka mpango wa akiba.
    - Niweke wapi Akiba?
    - Niweke Akiba au nikope?
    - Mkopo mzuri na mkopo mbaya
    - Kuepuka madeni makubwa kupita kiasi.
    - kwanini nikope?
    - Kuishi bajeti.
    - Malengo ya muda mrefu na muda.
    - Kuweka pesa kwenye shuguli inazozalisha.
    - Mfumo wa kifedha ni kwaajili ya watu wote.
    - Haki za mraji na majukumu yake.
    - Jambo gani la kufanya kabla ya kuchukua mikopo kwenye taasisi za kifedha.
    - Matatizo na njia za kutatua.
    - Kutambulishwa kwenye Bima na Mifuko ya hifadhi ya jamii.
    - Kutambulishwa kwenye huduma simu pesa.

2. Elimu ya Bima au Mfuko wa jamii kwa kikundi.Pamoja na umuhimu wakujiunga na mifuko ya bima na hifadhi ya jamii.
3. Vitabu vya HISA na elimu ya Hisa.
4. Ujasiliamali na uzalishaji mali.(IGA).
5. Riba nafuu.

**Village/Mtaa saving loans Association (M/VSLAs cycle).**



SUMBAWANGA MUNICIPAL COUNCIL

CERTIFICATE OF RECORGNITION OF A COMMUNITY BASED ORGANIZATION AND INCOME GENERATING ACTIVIES

I hereby certify that: (Name of CBO & IGA)

*Has been duly recognized under the council policy on community based Organizations (CBOs) with recognitions No: SMC/P.40/4/……*

*This certificate is to the following conditions/directions*

1. The organization shall operate within: Sumbawanga Municipal Council

2. The organization shall implement activities related to:

    - Help each other
    - Save and credit
    - Livestock keeping
    - Pottering

Issued this……..day of month, year

……………………………………………

UPENDO KIPESHA.

Coordinator of CSOs.

SUMBAWANGA MUNICIPAL COUNCIL.

(Coordinator seal)

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA

CHETI CHA KUTAMBULISHA KIKUNDI CHA KIJAMII.

Tunathibitisha kuwa:(kikundi cha…………) kimetambuliwa na sheria ya vikundi vya kijaamii kijamii kwa Namba:SMC/P.40/4…………

Cheti kinatolewa chini ya shuguli za kikundi na :

1. Kikundi kitafanya kazi zake ndani ya: SMC.
2. Kikundi kitafanya shuguli zifuatazo.
   - Kusaidia
   - Akiba na Mikopo.
   - Kilimo na ufugaji.

Tarehe: 30/03/2016

……………………………………………

UPENDO KIPESHA

Mratibu wa wa vikundi vya kijamii.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA.

……………………………………………………

(muhuri na sahihi ya mratibu wa vikundi)